# THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
# NATIONAL EXAMINATIONS COUNCIL
# CERTIFICATE OF SECONDARY EDUCATION EXAMINATION

**021** **KISWAHILI**

(Kwa Watahiniwa Wasiokuwa Shuleni tu)

**Muda: Saa 3** **Jumanne, 4 Oktoba 2011 mchana**

---

**Maelekezo**

1. Karatasi hii ina sehemu A, B, C, D na E.

2. Jibu maswali **yote** katika sehemu A, B na D, swali **moja (1)** kutoka sehemu C na maswali **matatu (3)** kutoka sehemu E. Swali la **15** ni la lazima.

3. Zingatia maagizo ya **kila sehemu** na ya **kila swali**.

4. Simu za mkononi **haziruhusiwi** katika chumba cha mtihani.

5. Vikokotozi **haviruhusiwi** ndani ya chumba cha mtihani.

6. Andika **Namba yako ya Mtihani** katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia.

Karatasi hii ina kurasa 5 zenye maandishi.

Find more free educational resources at http://maktaba.tetea.org

## SEHEMU A (Alama 10)

## UFAHAMU

Jibu maswali **yote** katika sehemu hii.

1. Soma kwa makini kifungu cha habari kifuatacho kisha jibu maswali yanayofuata:

Ndani, kama tulivyosema, **kiza totoro**! Hapana mmoja aliyemwona mwenziwe. Kunatisha! Na Najum, kidogo tu, kama asingaliogopa kuambiwa mwoga, angeghairi kwenda mbele. Si mahali pa kupita mtu. Vimulimuli vimetawanyika husema usiku wa manane, vinang'ara kama nyota za usiku usiotoka mbalamwezi, ila 'nyota' zile za mzimuni zilikuwa zinang'ara, kwa wakati ule, mchana, na zinazunguka huko na huko ndani ya mzimu, na wakati mwingine zilitaka hata kuingia katika macho ya wavulana wetu wawili majasiri. Kwa hiyo haistajabishi tukiona kuwa mwendo wao ulikuwa wa **kutayamamu** kama mwendo wa kaa wakienda kimbelembele na kibavubavu, wanapita na huku wanavikupua vile vimulimuli vilivyokuwa vinawajia usoni kila mara. Popo vile vile walikuwa wakiruka na kuwapiga mbawa zao usoni, kelele za komba na mabundi, waliokuwa hawana habari kama kumekucha zilikuwa zikiwazomea mwote walimokuwa wakipita.

Kwa mbali, inapata pima mia waliona baka moja jeupe jeupe lililotawanyika na kuchukua nafasi kubwa kidogo, na waliweza kukisia kuwa lile lilikuwa baka la jua; lakini kwa huku walioko halikufika hata kidogo anga lake.

Hapana aliyesema neno, wote wawili walikuwa wakienda kama mabubu – na hata hao mabubu nao wakati mwingine walikuwa **wakibobokwa.** Mara kwa mara Bwana Msa aliwasha kiberiti chake kumulika waendako, na wakiigundua njia watakwenda mpaka wakosee tena, na tena awashe kiberiti.

Baada ya kitambo, vimulimuli vilianza kupungua na mwendo wao, ingawa bado kiza, lakini ulikuwa haujambo kidogo. Walipoanza kulikaribia lile anga la jua, hata kiza nacho kilianza kukimbia kidogo kidogo.

Walipofika kunako lile anga la jua, waliona kuwa sehemu ile ya kichaka ilikuwa kidogo imetanzuka, kwa sababu miti ilipungua kuambatana; hapo walisimama kupumzika. Iliwachukua safari ya kiasi cha nusu saa hata wakafika pale. Bwana Msa alitia kidole katika tundu la mtembo wake, na alipokitoa, alikung'uta jivu juu ya kiatu chake, akaupuliza kwa nguvu kuzidi kusafisha. Kisha akatia **mnoga** wake, akawasha kiberiti. Upepo ulikuwa shwari, na moshi wote ulitanda hewani kwa muda kabla haujatanzuka, na harufu ya mnoga wake ilitosha kuwa **buhuri** ya kuufukiza 'Mzimu wa Watu wa Kale."

Baada ya kuvuta mara tatu nne, waliendelea na safari yao – sasa bila ya taabu kubwa; kwa hiyo, sasa ndio kwanza kila mmoja **alitafuta ulimi wake ulikokwenda**, na Bwana Msa aliugundua wake mbele. Bwana Msa aliuliza, "Mtu



Find more free educational resources at http://maktaba.tetea.org

akikaa kuchorachora upuzi tu, atachora kitu cha maana au kitu cha upuzi tu vile vile?" Lakini sauti yake alivyokuwa akisema bila ya kumtupia jicho sahibu yake, alionyesha kuwa anasema na nafsi yake tu kwa sauti. Kwa hakika hakutarajia jawabu la swali hili kwa Najum maana mara aliendelea mwenyewe kwa mwenyewe, ila sasa aligeuka kumtazama mwenziwe usoni. "Zipo sababu mbili zitakazokuzuia, Najum, kuniambia kwamba maneno yale yaliyoandikwa kwa Kiarabu katika karatasi ile ya Bwana Ali hayakuwa na maana kwa mwenyewe aliyeyaandika." Bwana Msa aliendelea kuvuta kiko chake kwanza akimwacha Najum yamwingie barabara maneno yake aliyoyasema. Halafu akaendelea, "Moja katika sababu hizo ni hii, kuandika stakabadhi ya mali mwenyewe, tena akawa nayo mwenyewe, asimpe mtu aliyemwuzia. Sababu ya pili hakutia sahihi yake wala tarehe alipoandika karatasi ile. Mambo mawili haya yatakuonyesha dhahiri kuwa ile karatasi ni kitu muhimu sana, wala haionyeshi kuwa Bwana Ali alikuwa kakaa kitako bana kazi akawa anachora tu."

Najum alitazama akaona sasa Bwana Msa anasema maneno ya upuzi, maana mambo mawili hayo aliyoyataja yanapingana yenyewe kwa yenyewe na yanarejea kule kule kuwa karatasi ile ni upuzi tu.

**Maswali**

(a) Eleza maana ya maneno yaliyokolezwa wino.
(b) Eleza mandhari ya habari hii.
(c) Kiongozi katika habari hii alikuwa ni mhusika mwenye wasifu gani?
(d) Unafikiri ni kwa sababu gani wahusika katika safari hii walitembea bila kuzungumza chochote?
(e) Eleza sababu mbili zilizomfanya Najum kusema kuwa mambo mawili aliyoyataja Bwana Msa yanapingana yenyewe kwa yenyewe.

2. Fupisha aya ya sita (6) ya habari uliyosoma kwa maneno yasiyozidi sabini (70).

## SEHEMU B (Alama 25)

## SARUFI NA UTUMIZI WA LUGHA

Jibu maswali **yote** katika sehemu hii.

3. Kwa kutumia mifano, eleza chanzo cha misimu na taja matumizi matatu (3) ya misimu.

4. Kwa kila tungo kati ya zifuatazo onesha kivumishi kisha bainisha aina ya kivumishi husika.
(a) Kikombe cha kaka kimevunjika
(b) Wachezaji wenu wanatafuta mpira
(c) Msichana mrembo anajikwatua
(d) Viatu vyote vimechafuka
(e) Wanafunzi wachache wamenunua vitabu.



Find more free educational resources at http://maktaba.tetea.org

5. "Lugha inapotumika vibaya huweza kupotosha lengo la msemaji." Fafanua ukweli wa usemi huu kwa mifano mitano (5).

6. Fafanua dhima ya 'ji' katika maneno yafuatayo:-
   (a) Jitu
   (b) Uzalishaji
   (c) Anajikwatua
   (d) Jicho.

7. Kwa kutumia mifano eleza maana ya
   (a) Kamusi wahidiya
   (b) Rejesta
   (c) Misemo
   (d) Lahaja
   (e) Lugha ya mazungumzo.

## SEHEMU C (Alama 10)

## UANDISHI

Jibu swali **moja (1)** kutoka sehemu hii.

8. Andika risala kwa niaba ya wenzako mnaomaliza Kidato cha Nne katika shule ya sekondari ya Kwedukwazu. Mgeni rasmi ni Afisa Elimu wa Mkoa.

9. Kwa niaba ya Shirika la Umeme Tanzania, andika tangazo kwenye gazeti la Mwananchi ukiwajulisha wananchi wa eneo la Yombo Dovya kuhusu tatizo la kukatika kwa umeme katika eneo lao siku ya tarehe 4/10/2011. Jina lako liwe Jimbi Tambitambi.

## SEHEMU D (Alama 10)

## MAENDELEO YA KISWAHILI

Jibu swali la **kumi (10).**

10. Kwa kutumia mifano mitatu (3) dhahiri, fafanua mfanano wa miundo ya Kiswahili na lugha nyingine za kibantu.



Find more free educational resources at http://maktaba.tetea.org

## SEHEMU E (Alama 45)

## FASIHI KWA UJUMLA

Jibu maswali **matatu (3)** kutoka sehemu hii. Swali la **15** ni la lazima

11. Semi zina vipera vyake. Fafanua vipera hivyo kwa kutoa mfano mmoja (1) kwa kila kipera.

12. "Falsafa na msimamo wa mwandishi ni nguzo muhimu katika kuijenga kazi yake." Jadili kauli hii kwa kutumia diwani teule mbili (2) kati ya zilizoorodheshwa. Toa hoja mbili (2) kwa kila diwani.

13. Jadili jinsi wahusika wakuu walivyotumika katika kukamilisha kazi za waandishi wawili (2) wa riwaya mbili (2) teule ulizosoma. Toa hoja tatu (3) kwa kila riwaya.

14. "Waandishi wa tamthiliya wameonesha migogoro na jitihada ya kuondokana na migogoro hiyo ili kuijenga jamii mpya". Jadili kauli hii ukitumia tamthiliya mbili (2) teule ulizosoma. Toa hoja tatu (3) kwa kila tamthiliya.

15. Eleza tofauti iliopo kati ya vigano na visasili. Toa mfano mmoja wa kisasili au wa kigano.

### ORODHA YA VITABU

**Ushairi**

| | | |
|---|---|---|
| Wasakatonge | - | M.S. Khatibu (DUP) |
| Malenga Wapya | - | TAKILUKI (DUP) |
| Mashairi ya Chekacheka | - | T.A. Mvungi (EP & D. LTD) |

**Riwaya**

| | | |
|---|---|---|
| Takadini | - | Ben Hanson (MBS) |
| Watoto wa Mama N'tilie | - | E. Mbogo (H.P) |
| Joka la Mdimu | - | A. J. Safari (H.P) |

**Tamthiliya**

| | | |
|---|---|---|
| Orodha | - | Steve Raynolds (MA) |
| Ngoswe Penzi Kitovu cha Uzembe | - | E. Semzaba (ESC) |
| Kilio Chetu | - | Medical Aid Foundation (TPH) |



Find more free educational resources at http://maktaba.tetea.org